



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA YA MUHEZA



**TAARIFA KWA UMMA**

**YAH: MTIHANI WA TAIFA WA KIDATO CHA NNE 2022.**

Mtihani wa Taifa wa kidato cha Nne umeanza rasmi siku ya Jumatatu tarehe **14/11/2022** ambapo wanafunzi wote wa **Kidato cha Nne** Nchini wanafanya mtihani huo wa kuhitimu elimu yao ya Sekondari (**O- LEVEL**) na unatarajiwa kukamilika mnamo **Desemba 01, 2022**.

Halmashauri ya Wilaya ya Muheza ni Miongoni mwa Halmashauri **11 za Mkoa wa Tanga** zinazofanya Mtihani wa Taifa wa kidato cha Nne.

Kwa upande wa Halmashauri ya Wilaya ya Muheza Jumla ya **Watahiniwa 2622** wameungano na watahiniwa wenzao nchini kufanya Mtihani huo wa kuhitimu Kidato cha Nne, miongoni mwao Wasichana ni **1485** na Wavulana ni **1137**.

Ikiwa Jumla ya Watahiniwa waliopo Shuleni tangu walipoanza kidato cha Kwanza 2019 hadi sasa 2022 ni **2535** kati yao Wasichana ni **1418** na **Wavulana wakiwa 1117**.

Sanjari na Watahiwa wa Shule, kuna Watahiniwa wa Kujitegemea '**Private Candidates**' (PC) wako **64** kati yao **Wasichana ni 45** na **Wavulana ni 19**.

Ambapo Watahiniwa wa **Maarifa (QT)** Jumla yao ni **23** wakiwemo **Wasichana 22** na Mvulana **01**

Aidha Jumla ya Shule za Sekondari zinazofanya Mtihani wa **Kidato cha Nne Mwaka huu wa 2022** Wilayani Muheza ni **29** kati ya hizo **24** ni za **Serikali** na Shule **5** za **Binafsi**.

Uongozi, Menejimenti na watumishi wote wa Halmashauri ya Wilaya ya Muheza wanawatakiwa Kila la kheri Watahiniwa wote wa **Mtihani wa kidato cha Nne kote Nchini** na kuwakumbusha wazingatie kanuni na taratibu zote za Mtihani.

*Kiope*

**KIOPE SIWEMA SALUM**

**KAIMU MKUU WA KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA MUHEZA.**

**15/11/2022**